**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**

TPHPA

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU USALAMA WA MBOGA ZA MAJANI NCHINI

**26 Machi, 2026**

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) inapenda kurejea Taarifa iliyochapishwa na Gazeti la kila siku la Nipashe Na. 0582351 la Tarehe 25/03/2026 lenye kichwa cha Habari, "**Mboga za majani zimesheheni sumu**", iliyonukuliwa kuandikwa na kuwasilishwa na Dkt. Jones Ackson Kapeleka.

Hata hivyo Mamlaka inakanusha kuwa yaliyochapishwa kwenye Gazeti la Nipashe sio matokeo ya utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) na wala sio mtazamo au msimamo wa Mamlaka wala wa Serilkali iliyokasimisha majukumu ya usimamizi wa Viuatilifu kwa TPHPA bali ni maoni binafsi. Mamlaka inapenda kufafanua kuwa mboga za majani zinazozalishwa na kuuzwa nchini **hazijasheheni sumu** kama ilivyoripotiwa.

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania inatambua kuwa katika kutumia Viuatilifu kudhibiti visumbufu vya mazao kunatokea ubakiaji wa

masalia ya viuatilifu kwenye mazao lakini sio kwa viwango hatarishi kama ilivyoelezwa kwenye Makala iliyochapishwa.

Kwa kutambua uwezekano wa kubaki kwa masalia ya Viuatilifu kwenye mazao, Mamlaka hufanya ufuatiliaji wa viwango vya masalia ya Viuatilifu (sumu) katika mazao ya chakula na mbogamboga nchini.

Mamlaka imekuwa ikichukua sampuli za mbogamboga na matunda mbalimbali kwa ajili ya uchambuzi wa kimaabara wa masalia ya Viuatilifu ili kulinda afya ya mlaji.

Katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Mamlaka imekusanya na kuchambua jumla ya **Sampuli 1300** za mbogamboga na matunda kutoka katika masoko makubwa na madogo katika mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Tanga, Mwanza, Singida, Tabora, Ruvuma, Shinyanga na Njombe, ambapo matokeo ya uchambuzi wa kimaabara yameonesha kuwa mboga na matunda hapa nchini hazina masalia ya viuatilifu (sumu) kwa viwango ambavyo ni hatarishi kwa afya ya walaji. Kazi hii ni endelevu katika masoko ya Mikoa yote nchini kila mwaka ili kulinda afya ya binadamu na mazingira.

Kutokana na mazao ya mbogamboga na mazao mengine kutokua na sumu, Mamlaka imendelea kuwezesha uuzwaji wa mazao hayo katika masoko ya kimataifa ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Februari 2026, kiasi cha **tani 2,481,051.92** cha mazao ziliweza kusafirishwa na kuuzwa nje ya nchi.
Aidha, Viuatilifu vyote vinavyotumika nchini ni vile vilivyosajiliwa na kuidhinishwa kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Mimea 2020. Aidha, katika kuhakikisha Viuatilifu vinavyotumika nchini vinakidhi vigezo vinavyotakiwa, Mamlaka imeendelea kufanya kaguzi za Viuatilifu vinavyouzwa na kutumika

nchini. Mamlaka inaendelea kusisitiza kuwa taarifa yoyote inayohusiana na shughuli zake zipatikane kupitia vyanzo sahihi.

Imetolewa na

Prof. Joseph C. Ndunguru

**MKURUGENZI MKUU**